

## **SHIDA YA MAJI TINGI KUWA HISTORIA**

Mradi wa maji katika kijiji cha Tingi unaotekelezwa na halmashauri ya wilaya ya nyasa mkoani Ruvuma unategemea kumaliza kero kubwa ya upatikanaji wa maji katika kijiji hicho.

Hayo yameelezwa na injinia wa maji wa Halmashauri ya nyasa Eng Evaristo Ngole wakati wa mkuutano wa hadhara wa wakazi wa kijiji hicho jana uliofanyika katika uwanja wa ofisi ya kijiji wakati akijibu kero za wananchi.

Injinia Ngole alifafanua kuwa Serikali imetoa kiasi cha shilingi 361,323,105/= kwa ajili ya mradi wa maji ulioanza kutekelezwa katika kijiji hicho na kwa sasa tayari chanzo kipyga cha maji kimeshajengwa na uchimbaji wa mtaro kutoka kwenye chanzo hadi kwenye tenki tayari kazi hiyo imeshafanyika.

Aliongeza kuwa kwa sasa maji yaliyopo hayatoshelezi mahitaji halisi hali iliyotakiwa waongeze chanzo kingine kipyga cha Ngumbo b ambacho kitatoa maji muda wote bila kukatika wala mgao au kusubiri yajae kwenye tenki ndipo yasambazwe kwa wananchi.

“Serikali imejipanga kumaliza kero ya maji katika kijiji hiki maji yaliyopo hayakuweza kuwafikia wote,ila ukishakamilika mradi huu shida ya maji itakuwa ni historia. Awali palikuwa na chanzo kimoja kinachosambaza maji lakini hayakutosheleza mahitaji ya wananchi wote wa kijiji cha Tingi ndio maana Serikali imeamua kujenga chanzo kingine kipyga ambacho kwa mwaka mzima kitatoa maji bila kukatika. alisema injinia wa maji ”.

Wananchi wa kijiji hicho waliipongeza serikali kwa kuwalizia kero ya maji katika kijiji hicho na kuahidi kuvilinda vyanzo hivyo vya maji vilivyo katika safu ya mlima ngumbo kwa kushirikiana na jumuiya ya watumiaji maji kijijni hapo.